

## Maswali

1. Yesu alipenda kwenda kuishi wapi?
2. Aliishi na nani?
3. Mbona Martha na Mariamu walipenda nyumba ikuwe safi na in'gare wakati Yesu alikuja?
4. Martha alikuwa akifanya nini?
5. Mariamu alikuwa akifanya nini?
6. Mbona Martha alikasirika?
7. Martha aliuliza Yesu afanye nini?
8. Yesu aliambia Martha nini?
9. Martha alifanya nini?
10. Tunaweza kusikiliza maneno ya Yesu namna gani?

## Majibu

1. Yesu alipenda kwenda kuishi Bethania.
2. Aliishi na Lazaro, Martha na Mariamu.
3. Kwa sababu Yesu alikuwa mgeni wa maana – Mwana wa Mungu.
4. Martha alikuwa na shughuli za kufanya usafi na kupika.
5. Mariamu alikuwa amekaa miguuni mwa Yesu akimsikiliza.
6. Kwa sababu alikuwa na shughuli nyingi na Mariamu hakumsaidia.
7. Martha alitaka Yesu aambie Mariamu akuje amsaidie.
8. Yesu alisema ilikuwa vyema kumsikilisika kuliko shughuli zingine.
9. Martha alikaa chini na akasikiliza Yesu.
10. Tunaweza kusikiliza maneno ya Yesu kwa kusoma Biblia.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1 Mwaka wa 3



# 44 Martha na Mariamu

## Marejeo

Luke 10: 38 – 42

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ni muhimu kusikiliza neno la Mungu kuliko kushughulika na mambo mengine

## Maneno maalum

- 44.1 Yesu + Bethania + Lazaro + Martha na Mariamu + pumzika + nyumba safi + mgeni wa maana + Mwana wa Mungu
- 44.2 Martha + shughulika + fanya usafi + pika
- 44.3 Mariamu + kaa karibu na Yesu + sikiliza kwa makini
- 44.4 Martha + shughuli nyingi + msalaba + Mariamu kaa bure + uliza Yesu + Mariamu saidia mimi + Mariamu sikiliza + kitu cha maana
- 44.5 Martha + wacha kazi + sikiliza Yesu + furahi +Biblia

**44.1** Yesu alipenda kwenda kwa kijiji cha Bethania kwa sababu marafiki zake Lazaro, Martha na Mariamu waliishi huko. Walimkaribisha Yesu vizuri sana nyumbani mwao. Yesu alikuwa amekuwa na kazi nyingi sana na alitazamia kwenda nyumbani kwao na apumzike kwa siku chache kule Bethania.

Martha na Mariamu walipenda nyumba yao kuwa safi ikiwa Yesu anakuja kwao kwa sababu alikuwa mgeni wa maana. Walijua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.



**44.2** Mariamu, Martha na Lazaro walimkaribisha na kuwa na furaha nyingi wakati Yesu alikuja nyumbani kwao. Martha alikuwa na shughuli nyingi sana. Alipanguza vumbi, akin'garisha na kufanya kila kitu kuwa safi bila mawaa. Yesu

alipofika na wanafunzi wake, Martha alianza kuwapikia chakula. Yesu na wanafunzi wake walikuwa ni wageni na walipikiwa.

**44.3** Mariamu alikaa karibu kwa miguu ya Yesu akimsikiliza. Yesu alikuwa akizungumza juu ya mambo mengi ya ajabu, na Mariamu alisikiliza kimakini sana. Alijua ni la maana kusikiliza kimakini kwa sababu Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa na mengi ya maana ya kusema.

**44.4** Mariamu alikuwa na jasho na kuzunguka. Alikimbia huku na kule kutengeneza chakula cha watu wote na alichoka sana. Alikasirikia Mariamu. Lazima aje anisaidie badala ya kukaa tu asifanye kitu!

Martha alienda kwa Yesu na akamwambia, "Ambia Mariamu aje anisaidie. Mimi nina shughulika na yeye amekaa tu kule bila kazi."



Lakini Yesu alisema, "Martha, Martha, ni vyema sana kuchukua wakati wako kutushughulikia kama nimekuja. Lakini nina mambo mengi ya maana kukwambia, ingekuwa vyema kama haungekuwa na hizo shuguli. Afadhali uwe na nafasi nyingi ya kusikiliza. Mariamu amechagua kitu cha maana cha kufanya."

**44.5** Kwa hivyo Martha aliacha kazi akapika chakula cha rahisi. Halafu wote wakakaa karibu na Yesu jioni yote ili wamsikilize. Yesu aliwambia juu ya Baba yake Mungu, aliyemzuri na mkarimu. Aliwambia vile Mungu alikuwa amemtuma ili watu wote wajifunze kumpenda Mungu na wapate kuokoka. Aliwambia juu ya Ufalme waajabu wa Mungu wenye Yesu atakuja nayo hivi karibuni kuusimamisha na pale kila mtu atafurahi.

Martha alifurahi kwa sababu alipata kusikiliza Yesu. Ninatamani kuwa mimi ndiye ningesikiliza Yesu usiku huo. Ninatumai hata wewe pia! Lakini, si hoja, kwa sababu tuna vitu vingi vyenye Yesu alifanya vyenye vimeandikwa kwa Biblia na tunaweza kusikiliza yaliyomo.